# MISINGI YA AGANO JIPYA: MWONGOZO WA KOZI

**Vitabu vya Injili**
**Kitabu cha Matendo ya Mitume**

## MAELEZO YA KOZI

Vitabu vitano vya kwanza vya Agano jipya ni vitabu muhimu vya Biblia kwa sababu vinasimulia maisha, mafundisho, kifo, na ufufuo wa Yesu, pamoja na mwanzo wa kanisa lake. Kila kitabu kimoja katika vitabu hivi vya Injili kina mtazamo wa kipekee na kusudi la kipekee. Katika somo la kwanza hadi la tano, kozi hii inaelezea usuli, muundo, yaliyomo, na mada kuu za kila Injili. Katika somo la sita hadi la nane, tutaangalia Kitabu cha Matendo ya Mitume, tukichunguza mambo makuu ya Luka alipokuwa akiandika na kutoa mfumo aliowapa wasomaji wake kama muktadha wa kuelewa mambo ya msingi na *mambo ya* upili. Kozi hii inategemea mfululizo wa video za Thirdmill, vitabu vya Injili na Kitabu cha Matendo ya Mitume  yaliyoandaliwa na Huduma ya Third Millennium na kuongozwa na Dkt. Pete Alwinson na Dkt. Hans F. Baker.

## MALENGO YA KOZI, MAKUSUDI NA ORODHA YA MODULI

### *Malengo*

Katika kozi hii, tunapenda kufikia malengo yafuatayo:

1. Tunatarajia kuwa utajifunza habari muhimu kuhusu usuli, yaliyomo, na mada kuu za kila kitabu cha Injili.
2. Tunatarajia kuwa utakuwa na hamu ya kumjua Yesu zaidi na kumfuata kwa uaminifu zaidi unaposoma habari njema.
3. Tunatarajia kuwa, utatumia mafunzo uliyojifunza katika Maisha yako unaposoma injili nne hasa kwamba, utamjua Yesu zaidi na kumfuata kwa uaminifu zaidi.
4. Tunatarajia kuwa utatumia nyenzo zote za kozi kujifunza mambo muhimu kuhusu usuli na maudhui ya Kitabu cha Matendo.
5. Tunatarajia kuwa utakuwa na shauku ya kufanya sehemu yako kusaidia kupanua ufalme wa Mungu ulimwenguni kote.
6. Tunatarajia kuwa utafanya mabadiliko fulani katika maisha yako kama mwitikio wa mafundisho  ya Kitabu cha Matendo, hasa ukifanya bidii zaidi kufanya sehemu yako katika upanuzi wa ufalme wa Mungu.

*Malengo*

Kwa kufanya mambo yafuatao, itakuwa ishara kuwa malengo yamefikiwa:

1. Kupata alama za kuridhisha katika mitihani na majaribio, kudhihirisha kuwa unaweza:
    - Kutambua taarifa muhimu kuhusu usuli wa kila injili nne, ikijumuisha mwandishi wake, hadhira, tarehe ya utuzi, na madhumuni.
    - Kutambua muundo na mambo muhimu yaliyomo katika kila moja ya injili nne.
    - Kutambua mada kuu za kila injili zote nne.
    - Kutambua taarifa muhimu kuhusu usuli muundo maudhui na mandhari ya kitabu cha Matendo.
2. Kamilisha miongozo ya masomo, ukieleza hisia zako kumwelekea Yesu na kupanuka kwa ufalme wa Mungu, na kuonesha jinsi umetumia mafundisho kozi hiyo katika maisha yako, hasa jinsi kozi hiyo imekusaidia kumjua Yesu vyema na kumfuata kwa uaminifu zaidi. Pamoja na njia ambazo Kitabu cha Matendo kimekuhimiza kufanya kazi ya upanuzi wa ufalme wa Mungu.

**Orodha ya Moduli za Kozi ya Misingi ya Agano Jipya.**

1. Utangulizi wa Vitabu vya Injili
2. Injili ya Mathayo
3. Injili ya Marko
4. Inili ya Luka
5. Injili ya Yohana
6. Usuli wa Kitabu cha Matendo
7. Muundo na maudhui ya Kitabu cha Matendo
8. Mada kuu katika kitabu cha Matendo

**MAELEZO KUHUSU VIPENGELE VYA KOZI**

*Beji*

1. Kila juma katika mazungumzo yenu mtatenga muda kwaajili ya kufanyia kazi vipengele vya Beji. Mwongozo huu wenye kurasa mbili utampa mkufunzi wenu mwongozo wa jumla wa namna mnavyotakiwa kuendeleza ujuzi huu muhimu katika huduma.

2. Katika wiki chache za mwanzoni, tumia muda wako ukiwa na kikundi chako pamoja na mkufunzi wako kupitia mada za kujadili kwenye maelezo ya beji.
3. Baada ya kuweka msingi imara kupitia majadiliano ya kikundi, tumia wiki zilizobaki kuifanyia kazi beji (mambo ya kufanya).
4. Utapatiwa beji pale mkufunzi wako atakapojiridhisha kuwa umetimiza vigezo vya beji kwa mujibu wa maelekezo yake.

***Moduli***

1. Jifunze kwa kutazama video, kusikiliza sauti, au kusoma nukuu.
2. Kamilisha mwongozo wa kujifunza kwa kila somo. Miongozo ya kujifunza itakuandaa wewe kujibu maswali ya mitihani, mazoezi ya kwenye mitandao na kukusaidia kuyatumia mafundisho ya somo katika maisha yako binafsi.
3. Fanya mitihani ya kila somo, mitihani itatolewa na mkufunzi wako. Mitihani inaweza kurudiwa kama kuna ulazima, tunapendekeza ufikie alama zaidi ya asilimia 80% kabla ya kushiriki mjadala wa wiki na kuhakikisha kuwa umeelewa maneno kwa usahihi.
4. Shiriki katika majadiliano ya kila wiki kwenye kundi lako pamoja na mkufunzi wako, mkitumia miongozo kuhusu kozi na uwezo wa kutumia maneno kwa usahihi katika maisha yako au huduma yako. Tunapendekeza mijadala kupitia video isiwe chini ya saa limoja

***Mtihani wa mwisho***

Unaweza ukafanya majaribio zaidi ya mara moja kama ukihitaji kujipima, lakini unatakiwa ujifunze na kusubiri kwa muda wa saa moja kabla ya kufanya jaribio jingine. Alama yako rasmi itakuwa ile uliyofanya vizuri zaidi kwenye majaribio yako na tunapendekeza upate zaidi ya 80% kabla ya kuendelea na kozi inayofuata.

**ALAMA ZA UFAULU**

Daraja la mwisho la ufaulu litahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Majaribio ya darasani yatakuwa na alama 30 kila moja.
2. Mtihani wa mwisho utakuwa na alama 100.
3. Ripoti ya beji ya maombi haiwezi kubadilisha daraja lako lakini ni lazima ipitishwe na mkufunzi ili uwe umekamilisha kozi.

*Alama za jumla katika kozi zinazozidi 80% zinahesabiwa kuwa ni ufaulu.*

------------------------------------

**Walioshiriki Kuandaa Kozi hii**

**Dk. Pete Alwinson** ndiye mchungaji mwanzilishi wa Willow Creek Church, PCA, Winter Springs, FL, ambapo alihudumu kama Mchungaji Mkuu kwa miaka 26.

**Dk. Richard J. Bauckham** ni msomi na mwandishi wa Agano Jipya na ni Profesa Mstaafu katika Chuo Kikuu cha St. Andrews huko Scotland.

**Dk. David R. Bauer** Ni Mkuu wa Shule ya Ufafanuzi wa Kibiblia na Ralph Waldo Beeson Profesa wa Mafunzo kwa Fatasi ya Bihoia katika Seminari ya Theoloja ya Asbury.

**Dk. Hans F. Bayer** ni Profesa wa Agano Jipya na Mwenyekiti wa Idara ya Agano Jipya katika seminari ya Theolojia ya Agano huko semina ya St. Louis, Missouri.

**Dk. Steve Blakemore** ni Profesa Msaidizi wa Falsafa katika Semina ya Biblia ya Wesley.

**Dk. Stephen Chan** ni Profesa Mshiriki wa Theolojia na Mafunzo ya Kidini katika Chuo Kikuu cha Seattle katika Jimbo la Washington.

**Dk. Peter Chow** ni Raisi wa Seminari ya Kiinjili ya China nchini Taiwan.

**Kasisi. Larry Cockrell** ni Mchungaji Mkuu wa Kanisa la Household of Faith na Mshiriki wa kitivo cha Seminari ya Kitheolojia ya Birmingham, Alabama.

**Dk. Steve Cowan** ni Mkurugenzi Mshiriki wa Kituo cha Rasilimali cha Apologetics na Profesa Mshiriki wa Falsafa na Apologetics katika Seminari ya Kitheolojia ya Birmingham huko Birmingham, Alabama

**Dk. Brandon D. Crowe** ni Profesa Msaidizi wa Agano Jipya katika Seminari ya Kitheolojia ya Westminister.

**Dk. Saul Cruz** ni Mwanasaikolojia, yeye na kewe, Pilar Cruiz-Ramos, ni wakurugenzi-mwenza wa Huduma za Armonia huko Jiji la Mexico

**Dk. Daniel Doriani** ni Makamu wa Rais wa Mikakati ya Kitaaluma na Profesa wa Theolojia katika semina ya Theolojia ya Agano

**Dk. John M. Frame** ni Profesa wa Theolojia na Falsafa ya Utaratibu katika Seminari ya Kitheolojia ya Reformed huko Orlando Florida.

**Dk. Matt Friedeman** ni Profesa wa Uinjilisti na Uanafunzi katika Seminari ya Biblia ya Wesley

**Dk. Mark Gignilliat** ni Profesa Mshiriki wa Uungu katika Agano la Kale katika Shule ya Beeson Di

**Kasisi. Michael J. Glodo** ni Profesa Mshiriki wa Masomo ya Biblia katika seminary ya Kitheoloja ya Reformed ya Orlando Campus.

**Dk. Jim Hamilton** ni Profesa Mshiriki wa Theoloja ya Kiblia katika seminari ya Theoloja ya Wabaptisti Kusini na Mchungaji Mhubiri wa Kanisa la Kenwood Baptist.

**Dk. Steve Harper** ndiye Makamu wa Raisi mwanzilishi wa Kampasi ya Florida Dunnam ya Seminari ya Kitheolojia ya Asbury

**Kasisi. Thad James, Jr.** ni Makamu wa Rais wa Mauala ya Kiakademia katika Seminari ya Kitholojia ya Birmingham huko Birmngham, Alabama.

**Dk. Riad Kassis** ni Mkurugenzi wa Mkoa kwa Baraza la Ng'ambo, huduma ya kimataifa ya mafunzo kwa viongozi wa Kikristo.

**Dk. Peter Kuzmic** ni Eva B. na Paul E. Toms Profesa Mashuhuri wa Misheni za Dunia na Masomo ya Ulaya katika Seminari ya Kitheolojia ya Gordon-Conwell na mwanzilishi mwenza na mkurugenzi wa seminari ya Kiinjii ya Kitheoloja huko Osijek, Kroatia

**Dr. David Lamb** ni Profesa Mshiriki wa Agano la Kale katika Seminari ya Theolojia ya Kiblia.

**Dk. Jeffery Lowmana** ni Mchungaji Mkuu katika Evangel Church PCA, huko Albaster Alabama, na Profesa wa Homeletics na Theolojia ya kumaliza katika seminari ya Kitheolojia ya Birmingham huko Birmingham, Alabama.

**Kasisi. Jim Maples** ni Mkugugenzi wa Programu ya Udaktari wa Huduma katika Uongozi wa Kichungaji katika Seminari ya Kitheolojia ya Birmingham huko Birmingham, Alabama

**Dk. John McKinley** ni Profesa Mshiriki wa Mafunzo ya Biblia na Theolojia katika Chuo Kikuu cha Biola.

**Dk. R. Albert Mohler, Jr.** ni Rais wa The Southern Baptist Theological seminary.

**Dk. WaiYee Ng** ni Profesa Mshiriki wa Masomo ya Kibiblia katika Shule ya Wahitimu wa Theolojia ya China huko Hong Kong.

**Dk. John Oswalt** ndiye Profesa mashuhuri wa Agano la Kale katika seminari ya Kitheolojia ya Asbury.

**Kasisi. Youssef Ourahmane** anahusika katika kuwafunza viongozi wa kanisa katika Shule ya Mafunzo ya Timotheo nchini Algeria.

**Dk. J. I. Packer** ni Profesa wa Theolojia ya Utaratibu na Kihistoria katika Chuo cha Regent huko Vancouver, British Columbia, na anahubiri na mihadhara kote nchini Uingereza na Amerika.

**Dk. Jonathan Pennington** ni Profesa Mshiriki wa Ufafanuzi wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia ya Wabaptisti Kusini.

**Dk. Gregory R. Perry** ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Mkurugenzi wa Initiative ya City Ministry katika Covenant Theological Seminary St. Louis, Missouri.

**Dk. Robert Plummer** ni Profesa Mshiriki wa Ufafanuzi wa Agano Jipya katika seminari ya Theolojia ya Wabaptisti Kusini.

**Dk. David Redelings** ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminari ya Betheli.

**Mr. Emad Sami** anahudumu katika Chuo cha Veritas kama Mkurugenzi wa Kanda ya Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini.

**Dk. Thomas Schreiner** ni James James Buchanan Harrison Profesa wa Ufafanuzi wa Agano Jipya na Mkuu Mshiriki wa Maandiko na Ufafanuzi katika Seminari ya Theoojia ya Southern Baptisti **Dk. Glen Scorgie** ni Profesa wa Theolojia katika Seminari ya Betheli ya Bethel Seminary's San Diego Campus.

**DK. James D. Smith III** ni Profesa Mshiriki wa Historia ya Kanisa katika Kampasi ya San Diego ya Seminari ya Betheli, na vile vile Profesa Msaidizi wa Dini katika Chuo Kikuu cha San Diego.

**Dk. Mark Strauss** ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminary ya Betheli ya San Diogo Campus. **Dk. Frank Thielman** ni Profesa wa Presbyterian wa Divinity in New Testament katika Beeson Divinity School.

**Dk. K. Erik Thoennes** ni Profesa wa Masomo ya Biblia na Theolojia katika Chuo Kikuu cha Biola. **Dk. Steven Tsoukalas** ni Profesa Mshiriki wa Apologetics na Mawazo ya Kikristo katika Semina ya Biblia ya Wesley

**Dk. Bill Ury** ni Profesa wa Theolojia ya Utaratibu na Kihistoria katika Seminari ya Biblia ya Wesley.

**Mch. kr. Simon Vibert** ni Kasisi wa zamani wa Kanisa la Mtakatifu Luka Wimbledon Park, Uingereza, na kwa sasa ni Makamu Mkuu wa Wycliffe Hall, Oxford, NA mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri.

**Dk. Brian Vickers** ni Profesa Mshiriki wa Ufafanuzi wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia ya Southern Baptist na Mhariri Msaidizi wa The Southern Baptist Journal of Theology.

**Mch. Dk. Peter Walker** ni Profesa wa Masomo ya Biblia kwenye Shule ya Huduma ya utatu (trinity).

**DK. Willie Wells** ni Mchungaji katika Kanisa la Pleasant Grove Baptist Church in Fairfield, Alabama na Profesa katika Seminari ya kitheolojia ya Birmingham huko Birmingham, Alabama.

**Dk. Stephen Wellum** ni Profesa wa Theolojia ya Kikristo katika Seminari ya Theolojia ya Wabaptisti Kusini.

**Dk. Ben Witherington III** ni Profesa wa masomo ya Ufafanuzi wa Agano Jipya katika Seminari ya Kitheolojia ya Asbury